# Zb 88(89) - Nitaimba milele

## Siku ya Mungu ya 13 - Mwaka A

Toni Iragi K




1. Nitaimba milele wema wako, ee **Bwana,**
nitawajulisha wote uaminifu **wako.**
Umesema: wema wangu wadumu mi**lele:**
umesimika mbinguni uaminifu **wako.**

2. Heri taifa linalojua mashangi**lio,**
wanaendelea, ee Bwana, katika mwanga **wako**.
Wanafurahiwa na jina lako mchana **kutwa,**
nao kwa haki yako wanajitu**kuza.**

3. Kwa maana Wewe ni nguvu yao tu**kufu,**
na kwa fazili yako unainua pembe **yetu**.
Maana ngao yetu ni yake **Bwana,**
na mfalme wetu ni wake Mtakatifu wa Isra**eli.**